2001537

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# KPSEA 2023

## 602

# KISWAHILI

## LUGHA

### Okt. 2023 — Muda: Saa 1

---

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA (Soma maagizo yafuatayo kwa makini)**

1. Umepewa kijitabu hiki cha Kiswahili na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 30. Jibu maswali yote.
2. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo:

   **NAMBA YAKO YA TATHMINI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
   **JINA LA SOMO**

5. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
6. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
7. Kwa kila swali 1 - 30 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
8. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora **KISTARI** katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano**
   **Katika kijitabu cha maswali:**
   28. Chagua jibu sahihi
   Mchicha huupatia mwili vitamini, ugali huupatia mwili
   A. protini.
   B. madini.
   C. kinga.
   D. wanga.

   Jibu sahihi ni **D.**
   **Katika karatasi ya majibu:**

   28. [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **28**, kisanduku chenye herufi D ndicho kilichochorwa kistari.

9. Chora kistari chako vizuri. **KISTARI** chako **LAZIMA kiwe cheusi** na kisijitokeze nje ya kisanduku.
10. Kwa kila swali, chora **KISTARI** katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

© 2023 The Kenya National Examinations Council



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

**Swali la 1 hadi la 5**
*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

*(Ni jioni. Leni na Kibo wamekutana mtoni. Ni msimu wa kiangazi.)*

**Leni :** *(Akitabasamu.)* Bingwa, hujambo? Ha! Ha! Ha! Umejitwika mtungi kichwani kutafuta maji!
**Kibo:** *(Akionyesha kukasirika.)* Sijambo, lakini mimi si bingwa. Ubingwa gani na hata tone la maji sina?
**Leni:** Samahani kaka. Sikudhani unaweza kukosa maji. Ajabu! Matangi yako makubwa yamekauka?
**Kibo:** Bila shaka. Unavyoona kiangazi kimetuathiri sisi sote. Hali ya anga isipobadilika tutaangamia.
**Leni:** *(Akionyesha kuhuzunika.)* Ni kweli unavyosema mwenzangu. Lakini hiyo anga itabadilikaje ilhali miti inakatwa ovyo?
**Kibo:** Ipo haja ya sisi kushirikiana ili kutunza na kuhifadhi mazingira yetu. Kumbuka tusipoziba ufa...
**Leni:** *(Akikubaliana naye.)* Tutajenga ukuta. Nasikitika hali hii ikiendelea tutakosa chakula. Wanyama na ndege nao watakosa makao.
**Kibo:** **Mwandani** wangu, hakika utunzi wa mazingira ni wajibu wetu.
**Leni:** Kweli kabisa. *(Wanaagana na kuondoka)*

1. Leni alimwamkua Kibo, hujambo? Ni salamu gani nyingine ambayo Leni angetumia kumwamkua Kibo?
   A. Chewa?
   B. Masalkheri?
   C. Sabalkheri?
   D. Shikamoo?

2. Leni alitumia lugha ya adabu alipokuwa akizungumza na Kibo. Chagua kauli aliyoitumia inayoonyesha adabu.
   A. Umejitwika mtungi kichwani kutafuta maji!
   B. Wanyama na ndege nao watakosa makao.
   C. Matangi yako makubwa yamekauka?
   D. Ni kweli unavyosema mwenzangu.

3. Katika mazungumzo, msikilizaji anaweza kukamilisha kauli ya anayezungumza. Chagua kauli iliyotumiwa kukamilisha nyingine katika mazungumzo haya.
   A. Bila shaka.
   B. Tutajenga ukuta.
   C. Kweli kabisa.
   D. Samahani kaka.

4. Leni alimweleza Kibo athari za kutotunza mazingira. Ungekuwa Kibo, ungetaja athari gani nyingine?
   A. Kiwango cha joto kuongezeka.
   B. Wanafunzi kuacha shule.
   C. Mahusiano baina ya watu yataharibika.
   D. Vyombo vya usafiri wa umma vitapungua.

5. Neno **mwandani** limetumika katika mazungumzo. Chagua neno lenye maana sawa na **mwandani**.
   A. Ndugu.
   B. Jirani.
   C. Sahibu.
   D. Mwenza.

**Swali la 6 hadi la 9**
*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Ushuru ni malipo yanayotozwa na serikali kama ada ya kuingiza bidhaa ndani ya nchi au kuziuza nje ya nchi. Pia, ni ada inayotozwa raia kwa kuuza au kununua huduma mbalimbali. Nchi yetu hutegemea ushuru ambao wananchi hutozwa ili kuendesha shughuli zake.

Shirika lenye jukumu la kukusanya ushuru nchini Kenya ni Halmashauri ya Ukusanyaji Ushuru almaarufu KRA. Shirika hili limepewa mamlaka ya kikatiba kukusanya aina zote za ushuru: ushuru wa mapato, ushuru wa forodhani, ushuru kutokana na shughuli za kitalii na nyinginezo.

Serikali huandaa bajeti kila mwaka ili kuhakikisha matumizi yafaayo ya fedha. Bajeti huwa na makadirio ya mapato na mgao wa fedha kwa matumizi mbalimbali. Makadirio hayo husomwa bungeni na Waziri wa Hazina ya Kitaifa kisha **kuidhinishwa**.

Ni wajibu wa kila mwananchi kulipa ushuru ili taifa letu liweze kujitegemea. Tukifanya hivyo, tutaweza kupiga hatua kimaendeleo. Tutakuwa na miundomsingi bora, huduma nzuri za kimsingi kama vile afya na elimu na hata nafasi zaidi za ajira.



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

6. Kulingana na kifungu, maendeleo ya taifa hutegemea:
   A. bidhaa zinazouzwa.
   B. bajeti ya taifa.
   C. huduma za kimsingi.
   D. ushuru unaotozwa.

7. Kifungu kimeonyesha kuwa ni haki ya KRA kukusanya ushuru kwa sababu:
   A. bajeti huandaliwa kila mwaka.
   B. imepewa mamlaka kikatiba.
   C. ni muhimu kuhakikisha matumizi yafaayo ya fedha.
   D. bidhaa nyingi huuzwa ndani na nje ya nchi.

8. Miundomsingi ikiimarika:
   A. viwanda vya uzalishaji bidhaa vitaimarika.
   B. wakulima watapata mazao mengi.
   C. idadi ya watu itaongezeka.
   D. uharibifu wa mazingira utapungua.

9. Chagua maana ya neno **kuidhinishwa** kama lilivyotumiwa katika kifungu.
   A. kuwasilishwa.
   B. kuchunguzwa.
   C. kukubaliwa.
   D. kukamilika.

**Swali la 10 hadi la 12**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Likizo iliyopita nilitumia muda wangu wa mapumziko kumsaidia mlezi wangu **kuwatunza** mifugo wetu. Jambo hilo lilimfurahisha sana mlezi wangu akanizawidi ndama wa kike. Nilimpa ndama wangu jina, Simati.

Nilijitolea kwa hali na mali kumtunza Simati. Anapendeza kwa rangi yake nyeupe na madoa meusi. Matarajio yangu ni kwamba siku za usoni atapata ndama wake. Wakati huo utakapofika, nitamkama maziwa.

Maziwa nitakayoyapata nitayagawa kwa matumizi ya nyumbani na mengine nitayauza kwa usaidizi wa mlezi wangu. Hela nitakazopata kutokana na mauzo ya maziwa hayo, nitaziweka kama akiba kwani akiba haiozi.

10. Kulingana na kifungu, msimulizi alipewa zawadi kwa sababu:
    A. alifika nyumbani kwa likizo.
    B. alimsaidia mlezi wake.
    C. alimpa ndama jina Simati.
    D. alitamani kuuza maziwa.

11. Chagua jibu linaloonyesha kuwa msimulizi anafahamu uwekezaji.
    A. Anatumia likizo yake vizuri.
    B. Anatarajia Simati atapata ndama.
    C. Anafurahisha sana mlezi wake.
    D. Anapanga kuuza maziwa ili apate pesa.

12. Msimulizi alimsaidia mlezi wake kuwatunza mifugo wao. **Kuwatunza** ni:
    A. kuwalinda.
    B. kuwatayarisha.
    C. kuwapenda.
    D. kuwafurahisha.

**Swali la 13 hadi la 15**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Kesho ni Ijumaa. Itakuwa sikukuu ya Mashujaa nchini. Kutakuwa na sherehe ya kuadhimisha siku hiyo. Jena na Joana watakariri shairi kuhusu mashujaa. Tangu juzi, wamekuwa wakifanya mazoezi ili kujiandaa. Mtondogoo watarejea shuleni. Watawasimulia wenzao kuhusu matukio ya siku hiyo.

13. Jena na Joana watarejea shuleni mtondogoo. Mtondogoo itakuwa siku gani?
    A. Jumamosi.
    B. Jumapili.
    C. Jumatatu.
    D. Jumanne.

14. Chagua vitendo vinavyoonyesha kuwa Jena na Joana wanapenda nchi yao.
    A. Kuhudhuria sherehe, kukariri shairi.
    B. Kurejea shuleni, kukariri shairi.
    C. Kusimulia matukio, kuhudhuria sherehe.
    D. Kusimulia matukio, kurejea shuleni.

15. Maana ya kujiandaa kulingana na kifungu ni:
    A. kujitambulisha.
    B. kujitayarisha.
    C. kujinufaisha.
    D. kujiburudisha.

2001537720015377 2001537720015377

*Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 16 hadi 20. Umepewa majibu* ***manne*** *hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Kuwa na afya yaani___16___bora ni jambo muhimu kwa binadamu. Mlezi wangu husema kuwa lishe bora na mazoezi ya viungo vya mwili ni njia___17___ya kutupatia afya njema. Yeye huhakikisha kwamba___18___: matunda, mboga, mihogo na maharagwe___19___wingi. Tukiwa na afya njema, tutaweza kufanya kazi kwa bidii kama___20___.

**16.** A. uhai B. nguvu C. kimo D. siha

**17.** A. kuzuri B. nzuri C. mzuri D. vizuri

**18.** A. tunakula B. tungekula C. tukila D. tulikula

**19.** A. ya B. kwa C. ni D. vya

**20.** A. kiwavi B. mchwa C. tausi D. njiwa

*Kutoka swali la 21 hadi la 30, chagua jibu sahihi.*

**21.** *Chagua umoja wa:*
**"Majembe yatatumiwa kupalilia mipapai yao michanga".**
A. Jembe litatumiwa kupalilia mipapai yake michanga.
B. Jembe litatumiwa kupalilia mipapai yake mchanga
C. Jembe litatumiwa kupalilia mpapai wake mchanga.
D. Jembe litatumiwa kupalilia mpapai wake michanga.

**22.** *Chagua jibu sahihi kujaza pengo.*
Jakaya amekuwa akiwasaidia____zamani.
A. hadi
B. kisha
C. tena
D. tangu

**23.** Ukitaka kwenda chooni utamwomba mwalimu ruhusa kwa kumwambia unataka kwenda _____
A. bafuni.
B. majifichoni.
C. msalani.
D. chumbani

**24.** Matu ni fundi wa nguo. Rinda la Anna limeshonwa na Matu. Kwa hivyo, Anna __________rinda na Matu.
A. wameshonewa
B. wameshonesha
C. ameshonewa
D. ameshonesha

**25.** *Chagua jibu sahihi kujaza nafasi.*
Mlango _____darasa ni safi.
A. za
B. ya
C. wa
D. la

**26.** Mjomba wako alikuletea zawadi juzi. Ikiwa leo ni Jumamosi, mjomba wako alikuletea zawadi siku gani?
A. Jumanne.
B. Jumatano.
C. Alhamisi.
D. Ijumaa.

**27.** Tamu ni kwa chungu ilhali mwepesi ni kwa:
A. mzito. B. mkubwa.
C. mnene. D. mpana.

**28.** *Chagua jibu linaloonyesha ukanusho wa sentensi ifuatayo:*
Munira amesoma kitabu hicho.
A. Munira hasomi kitabu hicho.
B. Munira hatasoma kitabu hicho.
C. Munira hakusoma kitabu hicho.
D. Munira hajasoma kitabu hicho.

**29.** Mtu anapomhimiza mwenzake kufanya kazi, tunasema anamtia shime. Je, mtu anapomsaidia mwenzake katika jambo fulani huwa:
A. anamfanyia hima.
B. anampiga jeki.
C. anachapa kazi.
D. anatia fora.

**30.** Katana na Kombo hawapendi kushirikiana na wenzao kufanya shughuli za vikundi darasani. *Chagua methali inayoweza kutumiwa kuwashauri kubadilisha tabia hii.*
A. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
B. Chelewa chelewa utakuta mwana si wako.
C. Mchagua jembe si mkulima.
D. Jifya moja haliinjiki chungu.

2001533772001533772001533772001533771